

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Baruapepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

Morogoro
02 Agosti, 2024

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan leo ameanza ziara rasmi ya kikazi mkoani Morogoro kwa kuzindua Hospitali ya Wilaya ya Gairo na kuzungumza na wananchi katika mkutano uliofanyika katika uwanja wa Shule ya Msingi Gairo.

Akizungumza na wananchi hao, Rais Dkt. Samia amewataka kuendelea kuzalisha zaidi mazao ya biashara na ya chakula.

Aidha, Rais Dkt. Samia amemtaka Waziri wa Kilimo kuangalia namna ya kuwasaidia wazalishaji wa zao la mbaazi kwa lengo la kuwawezesha kunufaika na bei bora zaidi.

Hali kadhalika, Rais Dkt. Samia pia amezindua Daraja la Berega lililopo Wilayani Kilosa ambalo linaunganisha Wilaya hiyo na Wilaya ya Kilindi Mkoani Tanga.

Vile vile, Rais Dkt. Samia amewataka wananchi wa Kilosa kutunza miundombinu ya Daraja hilo ili liwe chachu ya uchumi kwao na kuwaletea maendeleo.

Rais Dkt. Samia pia alizungumza na wananchi wa Dumila ambapo alisema kuwa Serikali inaendelea kuifanya kazi migogoro baina ya wakulima na wafugaji ambapo katika ziara yake Mkoani Morogoro atazindua kampeni maalum itakayojulikana kwa jina la **TUTUNZANE**.

Rais Dkt. Samia yuko Mkoani Morogoro kwa Ziara ya Kikazi kuanzia tarehe 2 - 6 Agosti, 2024.

Sharifa B. Nyanga
Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

